TANGAZO LA SERIKALI NA_____la tarehe _____

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA)

SURA YA 287

_____

SHERIA NDOGO

_____

(Zimetungwa chini ya kifungu cha 153)

_____

SHERIA NDOGO ZA (MAHUDHURIO YA LAZIMA NA UDHIBITI WA MIMBA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI) ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA MWAKA, 2017

Jina la tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za **(Mahudhurio ya lazima na Udhibiti wa Mimba katika Shule za Msingi na Sekondari)** za Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, 2017 na zitaanza kutumika tarehe zitakapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

Eneo la kutumika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Afisa Elimu" maana yake ni Mkuu wa Idara ya Elimu ya Msingi na Mkuu wa Idara ya Elimu ya Sekondari wa Halmashauri.

"Afisa Muidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi ikiwa ni pamoja na Maafisa Watendaji wa Mitaa na Maafisa Watendaji wa Kata wote.

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Iringa.

"Mamlaka inayohusika" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya, Serikali ya Kijiji au Kamati ya Maendeleo ya Kata.

"Mkurugenzi" Maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa ikiwa ni pamoja na Afisa yeyote anayekaimu Ofisi hiyo kwa maandishi akitekeleza majukumu ya Mkurugenzi.

"Mwanafunzi" maana yake ni mtoto aliyeandikishwa Shule na inajumuisha mtoto yeyote ambaye hajamaliza Elimu ya Msingi na; au Sekondari. Na ataendelea kuwa mwanafunzi hadi matokeo ya mtihani yatakapokuwa yametoka. Mtoto akiwa amefaulu bado ataendelea kuhesabika kuwa ni mwanafunzi.

"Mzazi" maana yake ni Baba au Mama wa mtoto aliyeandikishwa shule.

"Mlezi" Maana yake ni mtu yeyote mwenye dhamana ya kumtunza na kumlea mtoto au mwanafunzi huyo.

"Shule binafsi" maana yake ni shule zinazomilikiwa na mtu binafsi, shirika au taasisi binafsi na ambazo sio shule za serikali.

"Shule" maana yake ni Shule za Msingi na Sekondari zilizomo katika eneo la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Iringa

Kuandikishwa na mahudhurio

4. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kila mzazi au mlezi anao wajibu wa kisheria kuhakikisha mtoto wake mwenye umri wa miaka saba (7) anaandikishwa Shule ya Msingi kwa ajili ya Elimu ya Msingi au Mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya Sekondari anaandikishwa Shule na kuhudhuria masomo katika Shule hizo mpaka atakapomaliza masomo ya Elimu ya Msingi au Sekondari.

(2) Kila mwanafunzi aliyeandikishwa shuleni atahakikisha kuwa anahudhuria masomo kila siku za masomo hadi atakapohitimu katika hatua husika ya elimu kwa maana ya elimu ya msingi au sekondari.

(3) Litakuwa ni jukumu la Mzazi au Mlezi wa mwanafunzi aliyeamua kumpeleka mtoto wake katika Shule binafsi kutoa taarifa na uthibitisho wa maandishi mara moja katika ofisi za Mitaa na Kata kwa ajili ya kumbukumbu.

(4) Ni kosa kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi kwa Mzazi au Mlezi aliyempeleka mtoto wake shule binafsi kushindwa kutoa taarifa katika ofisi ya Kijiji au Kata kwa kumbukumbu.

Ukaguzi wa Elimu

5. (1) Afisa ELimu au Mkaguzi wa Shule kwa kushirikiana na Afisa Muidhiniwa wanaweza kwenda kwenye Shule yoyote na kufanya ukaguzi na kuhakikisha endapo matakwa ya Sheria ndogo hizi yanatekelezwa na Shule.

(2) Afisa Elimu au Mkaguzi wa Shule atawasilisha taarifa ya ukaguzi kwa mamlaka inayohusika ili hatua za kisheria ziweze kuchukuliwa dhidi ya watu wote watakaovunja Sheria Ndogo hizi.

(3) Mwanafunzi atakayekosa kuhudhuria masomo kwa siku tatu (3) mfululizo, au katika vipindi tofauti bila taarifa Shuleni atahesabika kuwa ni mtoro.

Mamlaka ya Afisa Muidhiniwa

6. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi, Afisa Muidhiniwa ndiye atakuwa mtekelezaji na msimamizi Mkuu wa Sheria Ndogo hizi katika eneo la Kijiji au Kata yake.

(2) Afisa Muidhiniwa ana mamlaka ya Kisheria kwa Mujibu wa Sheria Ndogo hizi, kufungua kesi na kusimama Mahakamani dhidi ya mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi.

Kazi na majukumu ya Kamati au Bodi ya Shule

7. (1) Majukumu ya Kamati au Bodi ya Shule yatakuwa kama ifuatavyo;-

(i) Kuhakikisha kuwa wanafunzi wote walioandikishwa Shule wanahudhuria masomo hadi watakapohitimu Elimu ya Msingi au Sekondari.

(ii) Kuhakikisha kuwa walimu wote waliopo katika Shule ya Msingi au Sekondari wanafundisha masomo yote waliyopangiwa kwa mujibu wa ratiba na maelekezo ya walimu wakuu au wakuu wa shule.

(iii) Kuhakikisha kuwa wanafunzi hawafanyishwi kazi za nje muda wa masomo.

(iv) Kuhakikisha kuwa wanatoa taarifa kwa maandishi ya wanafunzi watoro kwa mamlaka inayohusika ili kuchukua hatua zinazostahili.

Makosa kwa upande wa Mzazi au Mlezi

8. (1) Kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi itakuwa ni kosa kwa Mzazi au Mlezi au mtu yeyote :-

(i) Kushindwa kumwandikisha mtoto kuanza Elimu ya Msingi au kushindwa kumpeleka kidato cha kwanza mwanafunzi aliyechaguliwa kujiunga na Elimu ya Sekondari.

(ii) Kumkataza au kumzuia Mwanafunzi kuendelea na Elimu ya Msingi au Sekondari au kufanya jambo lolote litakalomfanya mwanafunzi ashindwe kuendelea na masomo yake.

(iii) Kumtuma Mwanafunzi kazi yoyote wakati wa masomo .

(iv) Kumuoza au kumwozesha Mwanafunzi au kusababisha kuolewa

(v) Kutompatia Mwanafunzi mahitaji ya msingi kama vile chakula, malazi, mavazi na vifaa vya shule.

(vi) Kutolipa kabisa au kutokulipa kwa wakati ada ya Shule na michango mingine muhimu iliyoamriwa na Kamati au Bodi ya Shule.

(vii) Kufanya majadiliano na mtu aliyesababisha mimba kwa binti yake ambaye ni Mwanafunzi kwa lengo la kuafikiana kirafiki.

(viii) Kushindwa kutoa taarifa ya ujauzito wa mwanafunzi ambaye ni mtoto wake.

(ix) Kushindwa kutoa taarifa shuleni juu ya mtoto wake ambaye hajahudhuria masomo kwa zaidi ya siku tatu mfululizo na yupo nyumbani.

Makosa kwa walimu

9. (1) Litakuwa ni kosa kwa mwalimu au mtu yeyote:-

(i) Kumsimamisha kuhudhuria Shule Mwanafunzi yeyote kwa kosa ambalo kimsingi halikusababishwa naye bali Mzazi/Mlezi wake au mtu yeyote.

(ii) Kumtumikisha Mwanafunzi kazi yoyote ambayo haikuwa katika mpango wa kazi za Shule na ambayo haijaidhinishwa na Kamati au Bodi ya Shule.

(iii) Kutoa adhabu zilizokatazwa chini ya Sheria yoyote, na Kanuni au Amri yoyote chini ya mamlaka yoyote husika.

(iv) Kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi

(v) Kumshawishi mwanafunzi kwa namna yoyote ile kwa lengo la kujihusisha na masuala ya mapenzi

(vi) Kukataa kwa makusudi au kushindwa, kukamilisha kipindi au vipindi alivyopangiwa kufundisha kwa siku hiyo au siku hizo.

Makosa kwa Jamii

10. Litakuwa ni kosa kwa mujibu wa Sheria hizi kwa mtu yeyote:-

(1) Kumwajiri Mwanafunzi kufanya kazi yoyote ile.

(2) Kumtorosha Mwanafunzi kabla ya kumaliza Elimu ya Shule ya Msingi na Sekondari.

(3) Kufanya mapenzi na Mwanafunzi au hata kumwandikia barua za mapenzi au kumshawishi kufanya naye mapenzi , kuacha kuendelea na masomo yake au kumtorosha Shule.

(4) Kumchumbia au kumuoa Mwanafunzi.

(5) Kumpa au kusababisha mimba kwa Mwanafunzi.

Makosa kwa mwanafunzi

11. (1) Litakuwa ni kosa kwa mwanafunzi;-

(i) Kutohudhuria Shule na; au masomo.

(ii) Kuwa au kukutwa na simu katika kipindi chote cha mihula ya Shule akiwa maeneo ya shule.

(iii) Kutoroka vipindi darasani.

(iv) Kuvunja taratibu za Shule husika.

(v) Kujihusisha na mapenzi wakati akiwa mwanafunzi

(2) Endapo mwanafunzi atapatikana na hatia ataadhibiwa kwa mujibu wa taratibu zinazosimamiwa na Kamati ya Nidhamu za Shule husika kwa kuzingatia Sheria ya Elimu Sura 353 na; au Sheria ya Mtoto, 2009.

12. (1) Mtu yeyote atakayevunja au kushindwa kutekeleza masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atahukumiwa kulipa faini isiyopungua shilingi elfu hamsini **(Tshs.50,000)** au kifungo kisichozidi miezi kumi na mbili jela au vyote kwa pamoja yaani faini na kifungo.

(2) Pamoja na adhabu itakayotolewa katika kifungu cha 12(1) hapo juu, mkosaji atawajibika kulipa gharama ambazo Halmashauri itakuwa imeingia kutokana na kukiuka masharti ya Sheria Ndogo hizi ikiwa ni pamoja na gharama za ukamataji.

Mhuri wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa umebandikwa katika sheria ndogo hizi kufuatia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika tarehe…….mwezi……2015 mbele ya ;

……
ROBERT MASUNYA
MKURUGENZI MTENDAJI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

……
STEPHEN MHAPA
MWENYEKITI HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA.

NAKUBALI

……
MHE. GEORGE B.SIMBACHAWENE (MB)
WAZIRI WA NCHI –OR-TAMISEMI

DODOMA,

TAREHE……..MWEZI……2017.